

Mnamo Feb, 2012 Mfungwa mmoja alilazwa katika Queen Elizabeth Hospital, kutoka na utumiaji wa madawa ulisababisha uvimbe katika mguu wake wa kulia chini ya goti.

Baada ya kupewa kitabu cha "Daktari Yesu" juu ya 18 Feb usiku alimuomba Bwana Yesu.

Siku iliofuata uvimbe wote ulitoweka na siku iliofuata akawa anatembea kama kawaida.

Miezi kadhaa iliyopita alipata tatizo lile lile katika mguu wake wa kushoto. Hospitali ile ile, dawa zile zile...uvimbe ulichukua miezi kadhaa.

Uvimbe katika mguu wa kulia ulichukua siku mbili. Yule mtu alisema tafauti ilikuwa ni maombi kwa Bwana Yesu

Wakati Maria alipokuwa mjamzito, mama mkwe wake akamwambia "kama utajifunguwa mtoto wa kike, basi mtoto wangu atakuacha."

Maria akawa na wasi wasi juu ya jambo lile na ikasababisha mtoto akazaliwa mgonjwa, ambae hauwezi kutibika. Padri akamwambia Maria omba, "**Tafadhali Yesu nisamehe mimi na Mama mkwe wangu.**" Na siku chache mtoto akapona.

Utusamehe hasa kwa wale ambao hawana mioyo au nia ya kuwasamehe sisi na huo ni ufunguo wa kuponya

Yesu, tafadhali nisaidie mimi kusamehe wale watu ambao hawana mioyo wa kuwasamehe mimi